

16C-Idghaam Al-Mutaqaaribayni (Zinazokaribiana)

3. إدغام المُتَقَارِبَيْنِ Idghaam Al-Mutaqaaribayni (Zinazokaribiana)

At-Taqaarub katika Tajwiyd ni kukaribiana herufi mbili katika makhraj na swiffah zao.

Taqaarub fil makhraj (kukaribiana katika makhraj) ni kuja herufi mbili kutoka katika kiungo kimoja kiasi cha kuwa hakuna makhraj inayozitenganisha baina yao; na kukaribiana katika swiffah. *Taqaarub fisw-swifah* (kukaribiana kwa swiffah) ni kuwafikiana herufi mbili katika swiffah zao kwa wingi.


إدغام المُتَقَارِبَيْنِ (Idghaam Al-Mutaqaaribayni) ni kuwepo herufi mbili ambazo zinakaribiana makhraj na swiffah. zenye kufuatana moja baada ya nyengine, herufi ya kwanza kuwa na sukuwn na ya pili huwa na *i'raab*, hapo huwajibika idghaam kwa kuingizwa herufi ya kwanza kwenye herufi ya pili.

إدغام المُتَقَارِبَيْنِ (Idghaam Al-Mutaqaaribayni) hutokea katika hali mbili:

Herufi za ق ك ل ر na mifano yake		
1. ق ك ¹		
Suwhah / Aayah	Matamshi	Mifano
Al-Mursalaat: (77: 20)	alam Nakhlu kk um mim-maaaaaim-mahiyn	أَلَمْ نَخْلُقْكُمْ مِنْ مَّاءٍ مَّهِينٍ
2. ل ر ²		
An-Nisaa (4: 158)	Barr afa'ahu-Allaahu Ilayhi	بَلْ رَفَعَهُ اللَّهُ إِلَيْهِ

¹Pekee katika Qur-aan

²Mara kadhaa katika Qur-aan

Twaahaa (20: 11)	wa qu R rabbi Zidniy 'ilmaa	 وَقُلْ رَبِّ زِدْنِي عِلْمًا
Al-Mutwaffifiyn (83: 14)	kallaa ba l raana 'alaa quluubihim ³	كَلَّا بَلْ رَانَ عَلَى قُلُوبِهِمْ

Hizo ni hali tatu za aina ya idghaam miongoni mwa nne ambazo zinagawanyika herufi zote za lugha ya Kiarabu; الْمُتَمَاتِلِينَ (Al-Mutamaathilayni), الْمُتَجَانِسِينَ (Al-Mutajaanisayni) na الْمُتَقَارِبِينَ (Al-Mutaqaaribayni).

Hali ya nne inajulikana kwa الْمُتَبَاعِدِينَ Al-Mutabaa'idayni (Zilizombali) kwa maana: Herufi mbili zinazofuatana, ambazo kila moja ina makhraj tofauti na swiffah yake tofauti kwa hivyo hazikufanana na hizo aina tatu za idghaam.

³Pekee kutokuifanya idghaam kutokana na السُّكُوت (Kipumziko). Rejea mlango wake